SWAHILI FORUM 12 (2005): 95-97

MAHOJIANO MAFUPI NA LUTZ DIEGNER JUU YA RIWAYA YA *BINA-ADAMU!*

KYALLO WADI WAMITILA

Kyallo Wadi Wamitila aliyezaliwa mwaka 1966 mjini Machakos nchini Kenya ni mwandishi anayeandika katika tanzu za ushairi, tamthilia, hadithi fupi na riwaya. Aidha, ameandika vitabu kadhaa vya watoto. Hadi hii leo amechapisha riwaya tatu. Riwaya zake *Nguvu ya Sala* (1999) na *Musaleo!* (2005) zilishinda Tuzo ya Fasihi ya Jomo Kenyatta mnamo 2001 na 2005. Katika mahojiano haya mafupi yaliyofanyika tarehe 03/11/2004 kwa njia ya baruapepe tulizungumzia riwaya yake ya pili *Bina-Adamu!* (2002). Riwaya hii ni juzuu ya kwanza ya trilojia ambayo imeendelezwa na *Musaleo!*. Juzuu ya tatu itaitwa *Pumzi za Kovu*. Hivi sasa mwandishi ni mhadhiri mkuu wa nadharia na fasihi ya Kiswahili katika Idara ya Kiswahili ya Chuo cha Elimu na Masomo ya Mbali cha Chuo Kikuu cha Nairobi. Ameandika vitabu vingi vya taaluma ya fasihi vikiwemo *Uhakiki wa Fasihi. Misingi na Vipengele Vyake* (2002), na *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia* (2003). Anaishi jijini Nairobi.

Lini na kwa nini ulipata mbegu ya kuandika* Bina-Adamu!*? Ulichukua muda gani kuiandika?

Nilipata msukumu wa kuandika *Bina-Adamu!* baada ya kuisoma riwaya ya Juan Rulfo ya *Pedro Paramo* na baada ya kufuatilia kwa makini siasa ya ulimwengu, ubepari na kusoma kuhusu utandawazi. Nilianza kuandika na kuimalizia huko Ujerumani nilipokuwa nikisoma Bayreuth (mwaka wa 1998-1999). Nadhani ilichukua mwaka mmoja kuandika.

Umekusudia kumfikia nani na riwaya ngumu kama hiyo?

Siamini kuwa hii ni riwaya ngumu nadhani inaeleweka. Nilikusudia isomwe na msomaji anaweza kuisoma.

Katika kumuumba mhusika msimulizi ulimchanganya na maisha yako kwa kiasi gani?

Uandishi wowote ule huwa na sifa ya kitawasifu (*autobiographical*). Mwenyewe nimefika Ujerumani na kwa kiasi lazima uzoefu wangu kuhusu historia ya huko na mambo mengine yalihusika hapa na pale lakini ni sehemu ndogo sana.

Tunaweza kusema kwamba mada kuu ya riwaya hiyo ni jinsi siasa ya Marekani inavyoutawala ulimwengu mzima unaowakilishwa kama kijiji. Umemchora P. P. ambaye ni kiongozi wa Marekani kama jitu mwenye sura ya kitoto, na mwishowe tunaambiwa kwamba jina lake ni ufupisho wa Peter Pan. Je, lengo lako kuu lilikuwa kuikosoa siasa ya Marekani au umekusudia zaidi kukosoa mfumo wa ubepari kwa ujumla?

Lengo langu lilikuwa ni kuukosoa mfumo wa ubepari na ubeberu kwa jumla. Marekani ni ishara iliyo wazi tu ya mfumo huo.

Inavyoelekea mhusika mkuu msimulizi anasafiri kwenye* axis *mbili. Kwanza anazuru sehemu mbalimbali za kijiji ambazo zinawakilisha nchi tofauti za dunia. Pili, anasafiri katika wakati. Kuhusu Ulaya na Japani tunarejeleshwa kwenye viongozi wa zamani Hitler, Churchill, De Gaulle, Franco, Stalin na Mfalme Hirohito. Ingawa majina hayo yanaweza kusomwa tu kama viwakilishi vya nchi zao, kwa nini hujatofautisha baina ya viongozi waliochaguliwa kidemokrasia na madikteta na waangamizaji?

Katika kuushambulia mfumo wa ubepari, utandawazi (hasa unaodhalilisha) na ubeberu sidhani kama tofauti kati ya wahusika wa kihistoria ni muhimu; muhimu ni ishara zinazofumbatwa na majina yao, siasa za nchi zao, na kadhalika. Unaweza kuwa Hitler bila ya kuwa Hitler, nadhani unanielewa. Ni muhimu kutaja kuwa saikolojia ambayo nimeisoma kwa kiasi fulani ina mchango mkubwa katika riwaya hii.

Tunaweza kusema kwamba ujumbe wa mwishoni mwa riwaya hiyo ni kumtambua P. P. kama jitu mpumbavu mwenye sura ya kitoto na kuacha kumhusudu. Unaonaje mtizamo huu?

Peter Pan ni kijana asiyekua. Marekani na nadhani mfumo wa kuandamizaji inaouwakilisha unafumbata jasira (*adventure*) ya aina fulani ambayo inahusishwa na majaribio ya watoto. Kisaikolojia unaweza kusema Marekani inasumbuliwa na *Peter Pan complex* (tanzo ya Peter Pan) – ndio maana nikatumia picha hii ambayo nadhani pia inaeleweka na wengi kutokana na nafasi ya hadithi hiyo.

Kuna sehemu kadhaa katika riwaya yako zinazodokeza hali ya nchini Kenya kama vile tabia ya viongozi na polisi, hali ya barabara na ujenzi, na kadhalika. Unaonaje mwenyewe nafasi ya madokezo hayo ya Kenya katika riwaya yako?

Riwaya ya mwandishi yeyote yule haina budi kuakisi (*reflect*) mazingira yake, siasa ya nchi yake na mambo yanayomhusu. Yapo mengi ambayo yanamkumbusha msomaji au kumgutusha (sijui!!) kuhusu nchi ya Kenya.

Swali lifuatalo ni refu lenye matawi matatu linalohusu mwingilianomatini:

1. Kwa mtizamo fulani, tunaweza kusema kwamba* Bina-Adamu! *ni kama maendelezo ya riwaya ya* Nagona *(1987/1990) ya Euphrase Kezilahabi. Bila ya kutaja vipengele vya mwingilianomatini kwa urefu, tunaweza kutoa mfano wa motifu ya safari inayounda fremu ya hadithi yenyewe. Unaonaje 'udugu' wa riwaya yako na ile ya Kezilahabi?

2. Katika sura ya ishirini tunasoma kuhusu kisa cha watu walioazima maguo ya jirani zao Washington, Churchill, Kaiser na Hirohito ambayo yanawapwaya. Msomaji anakumbuka mchezo wa kuigiza* Kaputula la Marx *(1978/1999) wa Kezilahabi. Jambo hili linaweza kusomwa kama dokezo la tashtiti la kwamba kuiga kwa ubepari kulikuwa na athari mbaya zaidi kuliko kuiga kwa usoshalisti kama kulivyooneshwa katika tamthiliya ya Kezilahabi. Unaonaje mtizamo huu?

3. Aidha kuna vipengele kadhaa vya mwingilianomatini wa riwaya hii na* Babu Alipofufuka *(2001) ya Said Ahmed Mohamed. Unaonaje 'udugu' wa riwaya yako na ile ya Said Ahmed Mohamed?

Kuhusu masuala ya mwingilianomatini nitasema kuwa ninavyojua *Bina-Adamu!* imetangulia *Babu Alipofufuka* kuandikwa. Nukuu ya T. S. Eliot inayotokeza katika riwaya hii inaweza kuwa sadifa.

Nagona niliisoma sana na kuiandikia tahakiki. Kama [*Bina-Adamu!*] ni riwaya inayoiendeleza hapo sijui kwa kuwa mitazamo na hasa teleolojia ya kazi zenyewe nahisi ni tofauti. Kuhusu motifu ya safari labda hali hii inatokana na matumizi ya motifu hii katika jasira na tendi (*epics*) za ulimwengu – eneo ambalo kama unavyojua nilifanyia utafiti wa PhD.

Nadhani maingiliano ya kazi zinazozungumzia maudhui yasiyokuwa mbali sana si ajabu. *Babu Alipofufuka* inachunguza suala la siasa ya Ulimwengu kwa kiasi kikubwa kama ilivyo *Bina-Adamu!*. Kazi zote ulizotaja zimewekewa msingi na fasihi simulizi za Kiafrika na kama unavyojua *"Oral literature is borderless"*. Maoni yako kuhusu kupwaya kwa maguo yanayotumiwa nadhani yanakubalika; uigaji wowote ule unakosolewa katika kitabu hiki.

Swali la mwisho ni lifuatalo: Unaonaje nafasi ya* Bina-Adamu! *katika uandishi wako kwa ujumla?

Nafasi ya *Bina-Adamu!* katika uandishi wangu sijui; nadhani wahakiki watajibu swali hilo. Kama nilivyodokeza nilitaka kuangalia suala la *'power'* katika ulimwengu na *'identity'* hali inayoendelezwa katika ngazi tofauti katika *Musaleo!* (bara) na *Pumzi za Kovu* (asasi ya ndoa).

Kwa kumalizia riwaya hii imetafsiriwa kwa Kirusi (na Mikhail Gromov) na sasa nina tafsiri yake ya Kiingereza ambayo tunafanya mpango wa kuhakikisha kuwa imechapishwa ili wasome wengine.

Nashukuru sana.